

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI NA MADINI**



**TAARIFA YA MAFANIKIO CHINI YA UONGOZI WA MHE.
SOSPETER MUHONGO (MB) KATIKA SEKTA NDOGO YA UMEME**

Disemba, 2014

A. MAFANIKIO

1. Kuongezeka kwa uzalishaji Umeme

Katika kipindi cha kuanzia 2012 hadi Julai 2014 kiasi cha umeme kinachozalishwa katika Gridi ya Taifa kiliongezeka hadi kufikia **MW 1396** ikilinganishwa na **MW 1220** za mwaka 2012. Ongezeko hili lilitokana na kukamilika kwa utekelezaji wa mradi wa kufua umeme kwa kutumia gesi asili wa **Ubungo II MW 105** na **Nyakato, Mwanza MW 60** unaotumia mafuta mazito.

Kufuatia hali mbaya ya maji kwa mitambo ya kufua umeme kwa kutumia maji, Serikali iliandaa mpango wa kuondoa mgawo kwa kuongeza uwezo wa kufua umeme wa **kiasi cha MW 572** kwa njia ya kukodi mitambo katika kipindi kifupi. Mkakati huo uliongeza kiasi cha **MW 422** kutokana na mitambo Symbion (MW 142), Aggreko (MW 100), IPTL (MW 80), na Mtambo wa TANESCO wa Gesi Asili wa Ubungo II (MW 100). Kutokana na **ughali wa mitambo ya kukodi**, Serikali ilianza kuratibu ujenzi wa mitambo yake ya kufua umeme kwa kutumia gesi asili ya Kinyerezi - I (MW 150) ambao uko mbioni kukamilika; Kinyerezi - II (MW 240) na Kinyerezi - III (MW 300) ambazo iko kwenye hatua mbalimbali ya majadiliano. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki ni pamoja na yafuatayo:

- (i) Kukamilika kwa mtambo wa MW 60 unaotumia mafuta mazito (*Heavy Fuel Oil*) Nyakato, Mwanza kuzinduliwa rasmi tarehe 8 Septemba, 2013.
- (ii) Kusainiwa kwa makubaliano ya Awali (*Memorandum of Understanding - MoU*) kati ya Serikali kupitia TANESCO na Kampuni ya China Power Investment (CPI) tarehe 16 Julai, 2013 kwa ajili ya ujenzi wa mtambo MW 600 - Kinyerezi III;
- (iii) Kukamilika kwa makubaliano ya ubia kati ya TANESCO (asilimia 40) na Kampuni China Power Investment – CPI (asilimia 60) katika mradi wa Kinyerezi III;

- (iv) Kusainiwa kwa makubaliano ya Awali (*Memorandum of Understanding - MoU*) kati ya Serikali kupitia TANESCO na Kampuni Poly Group ya China Mwezi Septemba, 2013 kwa ajili ya ujenzi wa mtambo MW 450 - Kinyerezi IV;
- (v) Kusainiwa kwa mikataba 35 ya utekelezaji wa Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini (*TurnKey Phase II*);
- (vi) Kuanzishwa kwa *Task Force* itakayohusika na uhamasishaji na ufuatiliaji wa matumizi bora ya maji (*Sustainable Water Management*) katika Mabonde ya Mtera na Pangani kwa lengo la kuwa na matumizi endelevu ya ufuaji umeme kwa kutumia nguvu za maji.
- (vii) **kupitishwa kwa Mkakati na Mwelekeo wa Kuboresha Sekta Ndogo ya Umeme Juni, 2014.** Lengo kuu la mkakati huo ni kuongeza ufanisi wa sekta ndogo ya umeme.

2. Kujenga na Kuimarisha Njia za Usafirishaji na Usambazaji Umeme

Hadi kufikia, mwaka 2011, zaidi ya asilimia 21 ya umeme uliokuwa unafuliwa ulikuwa unapotea kutokana na uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme. Serikali kupitia TANESCO ilianza mikakati ya **kukarabati na kujenga miundombinu** mipya ili kupunguza upotevu huo kwa lengo la kufikia wastani wa asilimia 19 ifikapo mwaka 2015. **Hadi Julai, 2014 lengo hili la asimilia 19 ya umeme lilikuwa limefikiwa.**

Aidha, mikakati hiyo ilipangwa kuendelea kufanyika katika mikoa mbalimbali nchini ambako Gridi ya Taifa inapita. Chanzo vya fedha ni pamoja na fedha za ndani pamoja na ufadhili kutoka Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la MCC la Marekani, Korea Kusini na shirika la JICA la Japan. Miradi iliyotekelezwa na inaendelea kutekelezwa ni pamoja na:

- (i) **Mradi wa Iringa - Shinyanga kV 400 (backbone).** Mradi huu uko kwenye ngazi ya utekelezaji.

- (ii) **Mradi wa Dar es Salaam – Chalinze – Tanga – Arusha (kV 400).** Mwezi Juni, 2012 TANESCO ilisaini mkataba wa marekebisho (*EPC addendum*) na mkandarasi, Kampuni ya TBEA ya China baada ya Serikali kuamua njia hiyo ianzie Dar es Salaama badala ya Morogoro. *Majadiliano kuhusu ufadhili yako kwenye hatua ya mwisho*
- (iii) **Mradi wa Makambako - Songea (kV 220).** Mwezi Agosti, 2011 TANESCO ilisaini mkataba na Kampuni ya SWECO ya Sweden kwa ajili ya kuandaa zabuni ya kumpata mkandarasi atakayesanifu na kutekeleza mradi. Tathmini ya fidia kwenye maeneo ambayo njia hiyo imekamilika. Aidha, mradi huo uliduruswa kutoka kV 132 mpaka kV 220 kutokana na kuwepo miradi mingi ya ufuaji umeme katika maeneo ambayo njia hiyo itapita ikiwemo Ngaka, Mchuchuma na Masigira.
- (iv) **Mradi wa Electricity – V.** Mradi huu unatekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na unahusisha usambazaji wa umeme katika vijiji, miji midogo na makao makuu ya wilaya katika Mikoa ya Geita (Bukombe), Magu na Kwimba (Mwanza) na Simiyu (Bariadi) na kukarabati vituo vikubwa vya kupozea umeme kwenye mikoa ya Dar es Salaam na Arusha. Kazi ya kujenga njia za umeme na vituo vya kupozea umeme itaanza katika Mwaka 2012/13.

3. Kuboresha Mifumo ya Umeme katika Jiji la Dar es Salaam

Kutokana na Jiji la Dar es Salaam kuwa kitovu uchumi wa Tanzania (economic hub), Wizara kupitia TANESCO katika kipindi husika ilianza mikakati ya kuimarisha miundombinu Jijini kwa kukarabati njia ya umeme kutoka Ilala mpaka Kurasini kwa kubadilisha waya kutoka milimita za mraba 150 hadi 432, kufunga transfoma za ukubwa wa MVA 15 katika vituo mbalimbali vya kupozea umeme, vikiwemo City Centre, Gongolamboto, Kigamboni, Kipawa, Kurasini, Mbagala, Mbezi Beach na Ubungo.

Aidha, kazi nyingine zinazoendelea ni ujenzi wa misingi ya nguzo kwa ajili ya njia ya umeme ya msongo wa kV 132 Jijini Dar es Salaam pamoja na vituo vya kupozea umeme, kV 132/33 vyenye

uwezo wa MVA 50 eneo la Gongolamboto (Factory Zone II) na Kipawa (Factory Zone III). Aidha, ujenzi wa kituo cha kupoeza umeme eneo la uwanja wa ndege wa Kimataifa Kilimanjaro (KIA) kV 132/33 chenye uwezo wa MVA 40 umekamilika. Kazi hizi zilifanyika chini ya Mradi wa TEDAP kwa udhamini wa Benki ya Dunia.

4. Kupunguza Gharama za Kuunganisha Umeme kwa Wateja

Ili kufikia lengo la kuwaunganishia umeme asilimia 30 ya watanzania ifikapo mwaka 2015, Serikali kupitia TANESCO, ilipunguza gharama za kuunganisha umeme wa njia moja (*single phase*) kwa wateja wadogo kwa wastani wa kati ya asilimia **30 na 77** kama ifuatavyo:

- a) Kwa wateja watakojengewa njia moja (*single phase*) kwenye umbali usiozidi mita 30 bila kuhitaji nguzo, katika maeneo ya vijijini watalipa **Shilingi 177,000** na wa mijini wanalipa Shilingi **320,960** badala ya **Shilingi 455,108** walizokuwa wakilipa hapo awali.
- b) Kwa wateja watakojengewa njia moja (*single phase*) na kuwekewa nguzo moja, katika maeneo ya vijijini ni Shilingi **337,740** na wa mijini ni Shilingi **515,618** badala ya **Shilingi 1,351,884** walizokuwa wakilipa hapo awali.
- c) Kwa wateja watakojengewa njia moja na kuwekewa nguzo mbili katika maeneo ya vijijini ni **Shilingi 454,654** na wa mijini ni Shilingi 696,670 badala ya Shilingi 2,001,422 walizokuwa wakilipa hapo awali.
- d) Kwa wakazi wa Lindi na Mtwara, Serikali kupitia REA ilitenga jumla ya Shilingi **bilioni 5** kwa mikoa ya Lindi (Shilingi **bilioni 2.88**) na Mtwara (Shilingi **bilioni 2.13**). Aidha, Serikali ilitenga Shilingi **bilioni 1.058** kwa kuboresha miundombinu ya umeme katika mkoa wa Lindi (Shilingi **milioni 500**) na Mtwara (**Shilingi milioni 558**).
- e) Kusaini **mikataba 35** na wakandarasi 16 wa kutekeleza Awamu ya Pili ya Mradi Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini katika mikoa mbalimbali Tanzania Bara.

- f) Kuanza na kuendendelea kufungwa mita maalumu zijulikanazo kama *smart meters* kwa watumiaji wakubwa wa umeme, utaratibu huo umesaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa wizi wa umeme na kuboresha makusanyo ya maduhuli ya TANESCO;
- g) **Kuondoa mgawo wa umeme** uliokuwa unaikumba nchi yetu mara kwa mara katika miaka ya hivi karibuni kuanzia mwezi Desemba, 2012;

5. Kuongeza Idadi ya Wateja

Wizara imefanikiwa kuongeza idadi ya Watanzania waliounganishiwa umeme (**connection level**) kutoka wateja 932,385 (**asilimia 18.4**) Mwaka 2011 hadi kufikia wateja takriban 1,300,000 (**asilimia 24**) mwaka 2014. Aidha, idadi ya watu waliofikiwa na huduma ya umeme (**access level**) iliongezeka na kufikia **asilimia 36** Mwezi Machi, 2014;

6. Ongezeko La Miundomimbinu ya Usafirishaji, Usambazaji Umeme

Katika kipindi husika Wizara kupitia TANESCO imeratibu na kukamilisha kufunga vipozea umeme (*transformers*) 8 vyenye uwezo wa MVA 15 katika vituo vya Bahari Beach, Gongolamboto, Kigamboni na Kunduchi; kufunga vipozea umeme viwili vyenye uwezo wa MVA 90 kila kimoja katika vituo vya Kipawa na Ubungo; na kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme nchini (kumaliza mgawo wa umeme) na hivyo kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

7. Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN)

Katika kipindi husika Wizara ilianza kutekeleza Miradi ya Kitaifa ya Kipaumbele chini ya Mfumo Mpya wa Ufuatiliaji na Tathmini unaolenga kuleta Matokeo Makubwa Sasa “**Big Results Now**”.

Tarehe 03 Julai, 2013 Wizara ilifanya uzinduzi rasmi wa utekelezaji wa Miradi hiyo ya Kipaumbele ya Kitaifa kwa kufanya **Maonesho ya Wazi (Open Day)** ya Sekta ya Nishati. Lengo likiwa ni Viongozi wa Wizara na wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara kuweka wazi ahadi kwa wananchi na jinsi Wizara ilivyojipanga

katika kutekeleza miradi hiyo. Jumla ya **miradi 29** ya Kitaifa ya Kipaumbele ilibainishwa kwa ajili kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia Mwaka 2013/14 hadi Mwaka 2015/16.

Aidha, Wizara ilianzisha kitengo maalumu (*Ministerial Delivery Unit - MDU*) cha kufuatilia utekelezaji wa miradi ya BRN katika Sekta ya Nishati ifuatavyo:

- (i) **Miradi saba (7) ya Kufua Umeme:** Mwanza - MW 60; Kinyerezi I – MW 150; Kinyerezi II – MW 240; Kinyerezi III – MW 300; Kinyerezi IV – MW 300; Singida Geo Wind Phase 1 – MW 50; na Kilwa Energy Phase 1 – MW 210;
- (ii) **Miradi ya (7) ya Kusafirisha Umeme:** Iringa-Shinyanga (Backbone) msongo wa kV 400; Dar – Arusha msongo wa kV 400; Singida - Arusha msongo wa kV 400; Makambako-Songea msongo wa kV 220; Somanga – Kinyerezi msongo wa kV 220; North West Grid Phase - I msongo wa kV 400; na Dar – Dodoma msongo wa kV 400.
- (iii) **Miradi (14)** ya usambazaji umeme katika mikoa mbalimbali nchini.
- (iv) **Mradi mmoja (1) wa Bomba la Gesi Asilia** kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam pamoja na mitambo miwili (2) ya kusafisha gesi hiyo katika maeneo ya Mnazi Bay - Madimba (Mtwara) na Kisiwa cha Songo Songo (Lindi).

8. Wakala wa Nishati Vijijini (REA)

Pamoja na juhudi nyingine, mafanikio ya kuongeza **access level** yametokana na utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini uliokuwa na miradi midogo **41** katika Mikoa **16 ya Tanzania Bara** (Arusha, Dodoma, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Pwani, Rukwa, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga). Kuanzia Mwezi Julai 2013 hadi Aprili 2014, wateja **wapya 15,817** walikuwa wameunganishiwa umeme kati ya **wateja 22,000** waliotarajiwa.

8.1 Upatinakanaji wa huduma za Mikoa ya Lindi a Mtwara

Wizara kupitia REA ilitekeleza jumla ya miradi 52 ya kusambaza umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2014 miradi 47, sawa na **asilimia 97** ilikamilika, ambapo wateja 1,925 waliunganishiwa umeme. Kati ya hao **wateja 1,135** ni kutoka Mkoa wa Lindi na wateja 790 ni kutoka Mkoa wa Mtwara. Serikali imepanga kukamilisha miradi mitano (5) iliyobaki katika mwaka 2014/15 wa fedha.

8.2 Idadi ya Makao Makuu yaliyopata Umeme

Katika kipindi husika, Wizara kupitia TANESCO imefanikiwa kupeleka umeme katika makao makuu ya wilaya za Utete, Kibondo na Kasulu, Ngorongoro na Loliondo.

9. Mikakati ya kuimarisha Sekta ya Nishati

Katika kukabiliana na changamoto mbalimbali za uimarishaji na utoaji wa huduma ya nishati katika Sekta ya Nishati, Wizara imeweka/inatekelezwa mikakati ifuatayo:-

- (a) Kuendelea kuboresha na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni katika sekta ya nishati.
- (b) Kuendelea kuongeza uzalishaji wa nishati kwa kutumia vyanzo mbalimbali ili kukidhi mahitaji na kuwa na akiba ya umeme (*reserve margin*) katika gridi ya Taifa.
- (c) Kuanzisha Mfuko wa Nishati (*Energy Fund*) utakaowezesha upatikanaji wa fedha zenye kukidhi utekelezaji miradi ya uzalishaji na usafirishaji kwa wakati kama ilivyobainishwa katika Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Umeme (PSMP).
- (d) Kushiriki kwenye biashara ya umeme kwa kuunganisha gridi ya Taifa na gridi za nchi jirani kupitia taasisi za *Southern Africa Power Pool (SAPP)* na *East Africa Power Pool (EAPP)*.

- (e) Kuimarisha mindombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme na hivyo kupunguza upotevu wa umeme.
- (f) Kuimarisha Mfuko wa Nishati Vijijini (REF) kwa kuongeza wigo wa vyanzo vitakavyochangia katika Mfuko kwa lengo la kuongeza kasi ya kupeleka umeme makao makuu ya wilaya zote na vijiji vingi zaidi.
- (g) Kuweka mazingira wezeshi ya ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji wa mafuta na gesi ili kupunguza bei ya mafuta kwa walaji kutokana na kupungua kwa gharama za usafirishaji, kurahisisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na biashara ya bidhaa za mafuta, na kupunguza uharibifu wa barabara;
- (h) Kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Mafuta ili kuwa na uhakika na usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini.
- (i) Kuendelea kuvutia wawekezaji zaidi katika utafutaji wa mafuta na gesi asili na kuhamasisha matumizi ya gesi hiyo majumbani, viwandani na taasisi mbalimbali ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.
- (j) Kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala na jadidifu; na matumizi bora ya nishati ili kutunza mazingira na kuokoa fedha.

B. HITIMISHO

Sekta za nishati ni miongoni mwa sekta muhimili katika kukuza na kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Ni matumaini ya Wizara kuwa kuendelea kushiriki kwa wadau katika utekelezaji wa sera, sheria na mikakati hiyo pamoja na mipango mingine ya kitaifa, kutaiwezesha Sekta ya Nishati kuendelea kuchangia zaidi katika maendeleo ya Taifa na kupunguza umaskini ili kukidhi matarajio ya Watanzania. Mwelekeo wa sekta hii ni kuhakikisha kuwa inachangia kwa kiwango kikubwa kwenye ukuaji na mipango ya maendeleo, kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya Watanzania. Hivyo, Wizara inadhamiria kuendelea kujiimarisha zaidi kiutendaji kwa lengo la kuzidi kuiimarisha sekta ili iweze

kutoa mchango stahiki kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

**BANGO KITITA LIONESHALO MUHTASARI WA MIRADI
MBALIMBALI ILIYOKAMILIKA NA INAYOENDELEA KATIKA
KIPINDI HUSIKA**

Mkoa	S/No.	Jina la Mradi	Scope of Works	Utekelezaji
MWANZA	1	NYAKATO Power station	<i>60MW Power Plant (Ufuaji)</i>	Imekamilika 2013
	2	NYASAKA Substation (NEW)	<ul style="list-style-type: none"> • 33/11kV; 1 x 10MVA • Transformer 4 x 11kV Feeder Bay (usambazaji)	Imekamilika 2013
	3	MABUKI substation (NEW)	<ul style="list-style-type: none"> • 220/132/33; 1x 45 MVA • 5 x 33kV Feeder Bays (Usafirishaji)	Imekamilika 2013
	4	MKUYUNI Substation (NEW)	<ul style="list-style-type: none"> • 33/11kV; 1 x 10MVA Transformer • 4 x 11kV Feeder Bay (Usambazaji)	Imekamilika 2013
	5	NYAKATO substation (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 1 x 33kV Feeder Bay (Usambazaji)	Imekamilika 2013
DODOMA	1	MZAKWE (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 33/11kV; 1 x 10MVA Transformer • 4 x 11kV Feeder Bay • Decommissioning Existing 2 x 2.5MVA 	Imekamilika 2013
	2	MNADANI (NEW)	<ul style="list-style-type: none"> • 33/11kV; 1 x 15MVA Transformer • 4 x 11kV Feeder Bay 	<i>Energized and loaded</i>
	3	KONDOA (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 1 x 33kV Feeder Bay 	<i>Energized and loaded</i>
	4	ZUZU (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 1 x 33kV Feeder Bay 	<i>Energized and loaded</i>
TANGA	1	KASIGA Substation (NEW)	<ul style="list-style-type: none"> • 1 x 132/33kV; 1 x 25MVA Transformer • 4 x 33kV Feeder Bay 	Imekamilika 2013
	2	KANGE Substation (NEW)	<ul style="list-style-type: none"> • 1 x 132/33kV; 1 x 25MVA Transformer • 4 x 33kV Feeder Bay 	Imekamilika 2013
	3	SAHARE Substation (NEW)	<ul style="list-style-type: none"> • 1 x 33/11kV; 1 x 15MVA Transformer • 3 x 11kV Feeder Bay 	Imekamilika 2013

Mkoa	S/No.	Jina la Mradi	Scope of Works	Utekelezaji
	4	SONGA (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 6 x 33kV Circuit Breakers 	Imekamilika 2013
MOROGORO	1	MSAMVU (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 1 x 220/33kV; 1 x 60MVA Transformer • 4 x 33kV Feeder Bay 	Imekamilika
	2	TANESCO OFFICE (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 1 x 33/11kV; 1 x 20MVA Transformer • 4 x 11kV Feeder Bay 	Imekamilika
	3	MIKUMI (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 1 x 33/11kV 1MVA Transformer • 2 x 11kV Feeder Bay 	Imekamilika
	4	TUNGI (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 1 x 33/11kV; 1 x 1MVA Transformer • 2 x 11kV Feeder Bays 	Imekamilika
	5	KIDATU (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • Replacement of Ifakara outdoor circuit breaker 	Imekamilika
	6	IFAKARA (New Voltage regulator)	<ul style="list-style-type: none"> • 33kV Voltage Regulator 15km from Ifakara towards Mahenge at Mavimba 	Inaendelea
IRINGA	1	TAGAMENDA (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 4 x 33kV Feeder including extension of busbar 	Imekamilika
	2	SABASABA (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 1 x 33/11kV; 1 x 5MVA Transformer • 5 x 33kV Feeder Bays • 3 x 11kV Feeder Bays 	Imekamilika 2013
MBEYA	1	MAFIATI (NEW)	<ul style="list-style-type: none"> • 1 x 33/11kV; 1 x 15MVA Transformer • 5 x 11kV Feeder Bays 	Imekamilika 2013
	2	IYUNGA (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • New control building • 4 x 33kV Feeder Bays • 6 x 11kV feeder Bays • Busbar and Sectionalisers 	Ujenzi unaendelea.
	3	MWAKIBETE (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 1 x 33kV Feeder Bay 	Imekamilika 2013
DAR ES SALAAM	1	UBUNGO (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 132kV GIS Switch gear • 1 x 132kV Feeder Bay • Extension of Busbar A & B • 132 KV Line to Zanzibar • New 132/33KV; 2x90MVA 	Imekamilika 2013 Imekamilika 2013

Mkoa	S/No.	Jina la Mradi	Scope of Works	Utekelezaji
			Transformers <ul style="list-style-type: none"> • Extended 33KV switchgears • Extended 11KV switchgears • Expanded SCADA system 	Imekamilika 2011
	2	KIPAWA	<ul style="list-style-type: none"> • 132/33KV; 2x 90 MVA new transformers • Upgrade of 33KV Busbar • 33/11KV; 1x15MVA • 132KV Line Bay for Factory Zone II 	Kazi hizi zinaendelea
	3	ILALA SUBSTATION	<ul style="list-style-type: none"> • 5, 33KV Breakers replaced with new ones • 3, 11KV Breakers supplied • 33/11kV; 1 x 15MVA transformer and its Circuit Breaker replaced by new • Replaced Metering and Alarm Panels 	Imekamilika 2013 Inaendelea
		SOKOINE SUBSTATION	<ul style="list-style-type: none"> • Addition of 1 x 15MVA, 33/11kV transformer. • Decommissioning of outdoor 33kV and 11kV switchgears and installation of new indoor switchgears and addition of feeders for more customers. 	Inaendelea Inaendelea
	4	VARIOUS SUBSTATION IMPROVEMENTS IN DAR ES SALAAM	<ul style="list-style-type: none"> • Addition of 12x15MVA transformers in Mbagala(1), Oysterbay(2), CityCentre(2), Kariakoo(1) Buguruni(I), Mbezi(1), GongolaMboto(1), Kigamboni(1), BahariBeach(1) 	Kazi zote zilimalizika 2012/13 isipokuwa Kigamboni na Bahari Beach
	5	TEGETA (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 2 x 132kV Feeder Bays • Busbar upgrade from 750A 	Imekamilika 2013

Mkoa	S/No.	Jina la Mradi	Scope of Works	Utekelezaji
			to 1250A	
	6	MAKUMBUSHO S/S	• Replacement of 33 KV cables	Imekamilika
	7	RAS KILOMONI (EXISTING)	• Submarine cable gantry and termination	Imekamilika 2013
	8	Distribution Substations in Dar es Salaam (Mburahati, Muhimbili, Oysterbay, Jangwani Beach)	• New Substations in these areas; 33/11KV; 2x15MVA transformers at each station	Inaendelea
	9	TRANSMISSION LINES IN Dar ES SALAAM	• Ubungo – Kurasini – Mbagala – Gongolamboto – Kipawa – Ubungo Transmission Line	Inaendelea
	10	CITY CENTRE SUBSTATION (132KV)	• Installation of a new 132/33KV substation at the City Centre	Inaendelea
COAST	1	MLANDIZI SUBSTATION (EXISTING) MSATA – BAGAMOYO; 33KV Line	<ul style="list-style-type: none"> • 132/33KV; 1x20MVA transformer • 1 Feeder Bay • Msata – Kiwangwa • Kiwangwa – Bagamoyo 	Imekamilika Kazi imekamilika kwa asilimia 90 Kazi imekamilika
K' NJARO	1	KIYUNGI Substation (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> • 132/66KV 1x20MVA; • 34km of 66KV transmission line from Kiyungi to Makuyuni • Construction of Control Building at Kiyungi • Construction of 132KV line from Kiyungi to Njiro Substation in Arusha 	Kazi imekamilika Kazi inaendelea Kazi inaendelea
	2	MAKUYUNI SUBSTATION (NEW)	• New 66/33 kV; 2x10 MVA; Makuyuni substation under JICA support.	Imekamilika
	3	KCMC Substation	• Installation of 33/11 kV; 1x10 MVA under JICA	Imekamilika

Mkoa	S/No.	Jina la Mradi	Scope of Works	Utekelezaji
		(NEW)	support	
	4	YMCA Substation (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> Expansion of the substation by installing 33/11KV; 1 x 17MVA 	Imekamilika
	5	LAWATE substation (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> Expansion of the substation by installing 33/11KV; 1x10MVA transformer 	Imekamilika
	6	BOMAMBUZI Substation (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> Expansion by adding 33/11KV; 1x15MVA transformer 	Inaendelea
	7	TRADING SCHOOL Substation (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> 33/11, 1x15MVA transformer Rehabilitation of the Trading school substation by installing 33KV switchgears One feeder Bay 5km 33kv line to the new KCMC substation 	Imekamilika
	8	KIA Substation (NEW)	<ul style="list-style-type: none"> 132/33KV, 2x20MVA transformers 6 x33KV feeders to feed KIA airport, USA River, Mandela University, Bomangombe, Mererani and Kiyungi. 	Imekamilika Inaendelea
ARUSHA	1	NJIRO Substation (EXISTING)	<ul style="list-style-type: none"> 132/33KV; 2x50MVA transformers Extension of 132kV and 33kV switch gears and addition of feeders for more customers. Installation of new digital substation control system based on IEC 61850. 	Inaendelea Inaendelea Inaendelea
	2	MOUNT MERU Substation (EXISTING)	132/33KV; 2x50MVA transformers	Inaendelea
	3	Kiltex Substation	<ul style="list-style-type: none"> 33/11; 1x15MVA transformer 	Inaendelea
	4	Njiro	<ul style="list-style-type: none"> 33/11; 1x15MVA 	Inaendelea

Mkoa	S/No.	Jina la Mradi	Scope of Works	Utekelezaji
		Substation	transformer	
	5	Sakina Substation	•33/11; 1x15MVA transformer	Inaendelea
	6	Themis Substation	•33/11; 1x15MVA transformer	Inaendelea
	7	Unga Limited	•33/11; 1x15MVA transformer	Inaendelea